# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

آياتها ٢٢ (٥٨) سُورَةُ الْمُجَادِلَةِ مَدَنِيَّةٌ (١٠٥) ركوعاتها ٣

*Ina Aya 22* **SURATUL MUJADILAH** *Ina Makara 3*

*(Imeteremka Madina)*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾

1. Mwenyezi Mungu amekwishasikia usemi wa mwanamke yule anayejadiliana nawe sababu ya mumewe, na anashtaki mbele ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنكُم مِّن نِّسَائِهِم مَّا هُنَّ أُمَّهَاتِهِمْ ۖ إِنْ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا اللَّائِي وَلَدْنَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ مُنكَرًا مِّنَ الْقَوْلِ وَزُورًا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَفُوٌّ غَفُورٌ ﴿٢﴾

2. Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama zao, (kwa hivyo wakajiepusha nao wasiwaingilie wala wasiwape ruhusa kuolewa na waume wengine); hao si mama zao. Hawakuwa Mama zao ila wale waliowazaa. Wanasema neno baya na la uwongo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye msamaha (na) Mwenye maghufira.

وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِن نِّسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَّا ۚ ذَٰلِكُمْ تُوعَظُونَ بِهِ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٣﴾

3. Na wale wawaitao wake zao mama zao, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, (wakataka kuwarejea wake zao wakae kama kidasturi ya mke na mume), basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana. Mnapewa maonyo kwa haya. Na Mwenyezi Mungu anajua (yote) mnayoyatenda.

فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَّا ۖ فَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ فَإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ۚ ذَٰلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤﴾

4. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza, basi awalishe maskini sitini (kila masikini kibaba kimoja cha chakula kinacholiwa sana katika mahala hapo). (Mumeambiwa) haya ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, (msipindukie); na kwa makafiri iko adhabu iumizayo.

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ كُبِتُوا كَمَا كُبِتَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ وَقَدْ أَنزَلْنَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۚ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٥﴾

5. Hakika wale wanaopinzana, (wanaokwenda kinyume) na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, watadhalilishwa kama walivyodhalilishwa wale waliotangulia. Na tumekwishateremsha Aya zilizowazi; na makafiri watapata adhabu ifedheheshayo.

1. Waarabu walikuwa na dasturi ya kutengana na mke kama akimwambia kuwa anamuona huyo mkewe kama mama yake. Basi huwa hakuachika na huyo mumewe wala haolewi na mtu mwingine, wala hana haki za mke kwa mumewe. Mwislamu mmoja alimwacha mkewe namna hii. Yule mke akanung unika kwa Mtume s.a.w. Basi dasturi hii ikavunjwa na dini ya Kiislamu.

6. Siku Mwenyezi Mungu atakapowafufua wote, awaambie yale waliyoyatenda; Mwenyezi Mungu ameyadhibiti, na wao wameyasahau; na Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا ۚ
أَحْصَاهُ اللَّهُ وَنَسُوهُ ۚ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ٦

7. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini? Haupatikani mnong'ono wa watu watatu ila yeye huwa ni wa nne wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao, wala wa wachache kuliko hao wala zaidi ila yeye huwa pamoja nao (kwa ujuzi wake), popote walipo; kisha siku ya Kiama atawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۖ
مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ
إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ
مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ
إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ٧

8. Huwaoni wale waliokatazwa kunong'onezana, kisha wakayarudia waliyokatazwa, na wananong'onezana juu ya mambo ya dhambi na ya jeuri na ya kumuasi Mtume? Na wafikapo kwako wanakuamkia kwa (maamkio) ambayo siyo maamkio aliyoamrisha Mwenyezi Mungu uwamkiwe kwa maamkio hayo, na husema katika nyoyo zao: "Mbona Mwenyezi Mungu hatuadhibu kwa haya tunayoyasema?" Basi (moto wa) Jahanamu utawatosha kuwatia adhabu; watauingia; napo ni mahali pabaya sana pa kurudia (kiumbe).

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نُهُوا عَنِ النَّجْوَىٰ ثُمَّ يَعُودُونَ
لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَيَتَنَاجَوْنَ بِالْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ
وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ
يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ وَيَقُولُونَ فِي أَنفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا
اللَّهُ بِمَا نَقُولُ ۚ حَسْبُهُمْ جَهَنَّمُ يَصْلَوْنَهَا ۖ فَبِئْسَ
الْمَصِيرُ ٨

9. Enyi mlioamini! Mnaponong'ona, (mnapozungumza) msinong'one, (msishauriane) juu ya mambo ya dhambi na jeuri na kumuasi Mtume, bali zungumzeni juu ya mambo ya kufanya wema na kuacha mabaya; na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwake mtakusanywa nyote.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا تَنَاجَيْتُمْ فَلَا تَتَنَاجَوْا بِالْإِثْمِ
وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ وَتَنَاجَوْا بِالْبِرِّ
وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ٩

10. Kwa yakini mazungumzo (mabaya) yanatokana na Shetani ili awahuzunishe wale walioamini, lakini (minong'onezano hiyo) haiwezi kuwadhuru chochote ila atake Mwenyezi Mungu. Waislamu wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

إِنَّمَا النَّجْوَىٰ مِنَ الشَّيْطَانِ لِيَحْزُنَ الَّذِينَ آمَنُوا
وَلَيْسَ بِضَارِّهِمْ شَيْئًا إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَعَلَى اللَّهِ
فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ١٠

11. Enyi mlioamini! Mnapoambiwa (katika mikutano) "Wafanyieni wasaa wenzenu katika (nafasi za) kukaa", wafanyieni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni nafasi (duniani na Akhera). Na (hata) ikisemwa, "Simameni", (ondokeni muwapishe wenzenu), basi ondokeni. Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa ilimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا فِي
الْمَجَالِسِ فَافْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ ۖ وَإِذَا قِيلَ
انشُزُوا فَانشُزُوا يَرْفَعِ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ
وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ
خَبِيرٌ ١١

---

8. Mayahudi walikuwa wakisema: *Sam Alaykum*, (yaani Mauti juu yenu); na huku wanaonyesha kuwa wanatamka *Salam Alaykum*, (Amani juu yenu na salama).

11. Makadiyani katika hii Aya waliyoifanya ya 12 wametia ushindani wao wa kupelekwa Nabii Isa mbinguni,

12. Enyi mlioamini! Mnapomsemeza Mtume toeni sadaka kabla ya kumsemeza (ili wapewe sadaka hizo masikini); hayo ni bora kwenu na ni ya kukusafisheni sana. Ikiwa hamkupata (cha kutoa), basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا نَٰجَيْتُمُ ٱلرَّسُولَ فَقَدِّمُوا۟
بَيْنَ يَدَىْ نَجْوَىٰكُمْ صَدَقَةً ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ
وَأَطْهَرُ ۚ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا۟ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

13. Oh! Mnaona tabu kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kumsemeza kwenu? Ikiwa hamjafanya haya basi. (Yamekwisha hayo). Na Mwenyezi Mungu amekusameheni. Basi simamisheni Sala na toeni Zaka na Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote.

ءَأَشْفَقْتُمْ أَن تُقَدِّمُوا۟ بَيْنَ يَدَىْ نَجْوَىٰكُمْ صَدَقَٰتٍ ۚ
فَإِذْ لَمْ تَفْعَلُوا۟ وَتَابَ ٱللَّهُ عَلَيْكُمْ فَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ
وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ ۚ وَٱللَّهُ خَبِيرٌۢ
بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٣﴾

14. Huwaoni wale (wanaojidai Uislamu, na) wamefanya urafiki na watu aliowakasirikia Mwenyezi Mungu? Hao si miongoni mwenu wala si miongoni mwao; (wanafanya unafiki tu) basi. Na huapa kwa uwongo, na hali ya kuwa wanajua (kuwa waongo).

أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِينَ تَوَلَّوْا۟ قَوْمًا غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِم
مَّا هُم مِّنكُمْ وَلَا مِنْهُمْ وَيَحْلِفُونَ عَلَى ٱلْكَذِبِ
وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٤﴾

15. Mwenyezi Mungu amewaandalia adhabu kali; kwa hakika waliyokuwa wakiyatenda ni mabaya kabisa.

أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ۖ إِنَّهُمْ سَآءَ مَا كَانُوا۟
يَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

16. Wamefanya viapo vyao (vya uwongo kuwa wao Waislamu) kuwa ngao (yao), wakaizuilia njia aliyoweka Mwenyezi Mungu basi itakuwa kwao adhabu ifedheheshayo.

ٱتَّخَذُوٓا۟ أَيْمَٰنَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا۟ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ
فَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿١٦﴾

17. Mali zao na watoto wao hawatawafaa kitu mbele ya Mwenyezi Mungu; hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.

لَّن تُغْنِىَ عَنْهُمْ أَمْوَٰلُهُمْ وَلَآ أَوْلَٰدُهُم مِّنَ ٱللَّهِ شَيْـًٔا ۚ
أُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿١٧﴾

---

wakasema katika kupoteza kwao: "Neno hili kurafiishwa lililotumiwa kwa ajili ya wa-aminio linaweza kuwaongoza wale wanaodhani kuwa kurufaishwa kwa Nabii Isa ni kupelekwa mbinguni . . ." Wameona Makadiyani kuwa katika kurafiishwa Nabii Isa Mwenyezi Mungu ametumia *Warafiukailayya* (= Nakuleta kwangu). Hapa imeandikwa: *"Yarfailahul Ladhyna Amanuu Minkum"* tupu, haikutiliwa kiongezaji cha kuonyesha kupelekwa mbinguni. Wanajua, lakini wanataka kupoteza watu kusudi.

Inataka watu watukuzane, wahishimiane, ndipo watakapopendana. Na Waislamu wote wanaamrishwa wapendane. Na katika yanayopelekea kupendana ni kuhishimiana. Na kuna watu kama hawa ambao lazima wapewe hishima yao, kama alivyosema Mtume:

(1) Mkubwa kwa umri;
(2) Mkubwa katika cheo cha dini;
(3) Mkubwa katika cheo cha kidunia
(4) Mwenye hishima kwa watu wote;
(5) Mwenye hishima kwa watu wake;
(6) Mwenye ihsani na wewe;
(7) Mwenye ihsani kwa viumbe wengine; na kama hawa. Anasema Mtume, katika Hadithi sahihi, kuwa kila mwenye haki apewe haki yake kamili.

Na ukimpa hishima mwenzako na aliye wake, na yeye atakupa hishima wewe na waliyo wako. Atakuwa yeye na watu wake wamefurahi na nyiye, na nyiye mumefurahi na wao. Basi yatapatikana mapenzi; na Mapenzi ni jambo kubwa kabisa litakiwalo. Na hishima tupu pasina kutimiziana haki haina taathira kubwa.

18. (Wakumbushe) Siku atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuapie (Mwenyezi Mungu kwa uwongo) kama wanavyoapa kwenu, na watadhani ya kwamba wamepata kitu (kwa kusema uwongo huo)! Kwa hakika hao ndio waongo hasa.

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿١٨﴾

19. Shetani amewatawalia, akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hao ndio kundi la Shetani. Sikilizeni! Kwa hakika kundi la Shetani ndilo lenye kuhasirika.

اسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ فَأَنسَاهُمْ ذِكْرَ اللَّهِ أُولَٰئِكَ حِزْبُ الشَّيْطَانِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٩﴾

20. Yakini wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa watakaodhalilika.

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَٰئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ ﴿٢٠﴾

21. Mwenyezi Mungu amekwishaandika (ya kuwa): "Bila shaka Nitashinda mimi na Mitume yangu!" Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾

22. Huwapati (huwaoni) watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, kuwa wanawapenda wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake; hata wakiwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio ambao (Mwenyezi Mungu) ameandika (amethibitisha kweli kweli) nyoyoni mwao imani na akawatia nguvu kwa Roho itokayo kwake; na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito mbele yake; humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi Naye. Hao ndio kundi la Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo linalofaulu.

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أُولَٰئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

آياتها ٢٤ (٥٩) سُورَةُ الْحَشْرِ مَدَنِيَّةٌ (١٠١) ركوعاتها ٣

*Ina Aya 24* *Ina Makara 3*

# SURATUL HASHR

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

سَبَّحَ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ①

2. Yeye ndiye aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu (Mayahudi wa Kibanin Nadhir) katika nyumba zao (huko Madina); wakati wa uhamisho (wao) wa kwanza. Hamkudhani ya kuwa watatoka, (kwa nguvu zao walizokuwa nazo Madina), nao walidhani ya kuwa ngome zao zitawalinda na (kufikwa na amri ya) Mwenyezi Mungu; lakini Mwenyezi Mungu aliwajia kwa mahali wasipopatazamia, na akatia woga katika nyoyo zao; (wasiweze kupigana na Waislamu walipokuja kupigana nao). Wakawa wanazivunja nyumba zao kwa mikono yao na kwa mikono ya Waislamu; basi enyi wenye macho, (maoni)! Zingatieni.

هُوَ الَّذِيْٓ أَخْرَجَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ أَهْلِ الْكِتٰبِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ ۚ مَا ظَنَنْتُمْ أَنْ يَّخْرُجُوْا وَظَنُّوْٓا أَنَّهُمْ مَّانِعَتُهُمْ حُصُوْنُهُمْ مِّنَ اللّٰهِ فَأَتٰىهُمُ اللّٰهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوْا ۚ وَقَذَفَ فِيْ قُلُوْبِهِمُ الرُّعْبَ يُخْرِبُوْنَ بُيُوْتَهُمْ بِأَيْدِيْهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِيْنَ ۚ فَاعْتَبِرُوْا يٰٓأُولِي الْأَبْصَارِ ②

3. Na lau kama Mwenyezi Mungu asingaliwaandikia uhamisho angaliwaadhibu hapa duniani (adhabu kubwa zaidi kuliko hii); na katika Akhera watapata adhabu ya Moto.

وَلَوْلَآ أَنْ كَتَبَ اللّٰهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ فِي الدُّنْيَا ۚ وَلَهُمْ فِي الْأٰخِرَةِ عَذَابُ النَّارِ ③

4. Hayo ni kwa sababu walimhalifu Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na anayemhalifu Mwenyezi Mungu (Mwenyezi Mungu humtesa tu), kwani Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

ذٰلِكَ بِأَنَّهُمْ شَآقُّوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ۚ وَمَنْ يُّشَآقِّ اللّٰهَ فَإِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ④

5. Mtende wo wote mlioukata (katika hicho kiambo cha Mayahudi) au mliouacha umesimama vile vile katika mashina yake; yote haya ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; (hapana lawama juu yenu); na kwa kuwadhalilisha wavunjao Sharia.

مَا قَطَعْتُمْ مِّنْ لِّيْنَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوْهَا قَآئِمَةً عَلٰٓى أُصُوْلِهَا فَبِإِذْنِ اللّٰهِ وَلِيُخْزِيَ الْفٰسِقِيْنَ ⑤

---

1. Sura hii inaitwa Kufukuza (kuhamisha), kwa sababu inaeleza habari za kufukuzwa kutoka Madina — kabila ya Kiyahudi iliyokuwa ikiitwa Banu Nadhiri.

2. Kutolewa kwa Mayahudi wa Banin Nadhir katika Madina kumeitwa "Uhamisho wa kwanza," kwa sababu baada ya hapa Mayahudi walihamishwa tena na kutolewa katika miji ya Kiarabu. "Uhamisho" wa mwisho ulikuwa katika zama za Sayyidna Umar alipowapa Amri Mayahudi wa Khaybari kutoka hapo Khaybari na kuguria Shamu.

6. Na mali aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwao hamkuyaendeshea mbio farasi wala ngamia (hamkuyaatabikia), lakini Mwenyezi Mungu huwapa mamlaka Mitume yake juu ya wowote awatakao (kama alivyokupeni hivi); na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

وَمَآ أَفَآءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ مِنْهُمْ فَمَآ أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ
مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يُسَلِّطُ رُسُلَهُۥ عَلَىٰ
مَن يَشَآءُ ۚ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝٦

7. Mali aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji (vilivyo karibu na Madina) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. (Basi yatatumika kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu), na kwa ajili ya Mtume (wake, basi atachukua mwenyewe) na jamaa (zake) na mayatima na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, ili wasiwe kinyang'anyiro baina ya matajiri wenu tu. Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na muogopeni Mwenyezi Mungu; kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

مَّآ أَفَآءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ
وَلِلرَّسُولِ وَلِذِى الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَٰمَىٰ وَالْمَسَٰكِينِ
وَابْنِ السَّبِيلِ كَىْ لَا يَكُونَ دُولَةًۢ بَيْنَ الْأَغْنِيَآءِ
مِنكُمْ ۚ وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ
عَنْهُ فَانتَهُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ
الْعِقَابِ ۝٧

8. (Basi) wapewe (mali hayo) mafakiri wa Kimuhajiri ambao walifukuzwa katika nyumba zao na mali zao; (wakakhiari kuwacha hayo) kwa ajili ya (kutafuta) fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi (yake) na kuinusuru (dini ya) Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi hao ndio Waislamu wa kweli.

لِلْفُقَرَآءِ الْمُهَٰجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِن دِيَٰرِهِمْ
وَأَمْوَٰلِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَٰنًا
وَيَنصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُولَٰٓئِكَ هُمُ
الصَّٰدِقُونَ ۝٨

9. Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (yaani Madina) na wakautakasa Uislamu (wao barabara) kabla ya (kuja) hao (Muhajiri huko Madina) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao Muhajiri), na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli.

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُو الدَّارَ وَالْإِيمَٰنَ مِن قَبْلِهِمْ
يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ
حَاجَةً مِّمَّآ أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ
كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ
فَأُولَٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ۝٩

10. Na (kadhalika wapewe mali hayo Waislamu) waliokuja baada yao (wakawa wanapendana na Waislamu waliotangulia, wanawaombea dua) wanasema: "Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia (kufa) katika Uislamu. Wala usijaaliye katika nyoyo zetu

وَالَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ
لَنَا وَلِإِخْوَٰنِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَٰنِ وَلَا
تَجْعَلْ فِى قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا

6-7. Inatajwa namna ya kugawiwa ngawira (nyara). Sio kugawiwa wale wapiganaji tu au kuchukuwa wakubwa tu, wakipigana wasipigane. Sivyo hivyo. Ikiwa hivyo itakuwa ni kinyang'anyiro baina ya matajiri tu—masikini wasalie katika ule ule tu umasikini wao. Na sivyo hivi unavyotaka Uislamu. Uislamu unataka uwaondoshee viumbe vyote uhitaji na ufakiri, kwa njia ya taratibu na nzuri — taratibu ndio mwendo.

8-9. Zinatajwa sifa za Muhajiri na Ansari.

10. Zinatajwa sifa ya Waislamu wema — nayo ni kutokuwa na mifundo na uadui na uhasidi na kama haya

undani kuwafanyia Waislamu (wenzetu) Mola wetu! Hakika Wewe ni Mpole sana, Mwenye rehema mno."

11. Huwaoni wale wanafiki wanawaambia ndugu zao walio makafiri miongoni mwa watu waliopewa Kitabu (kabla yenu) Mayahudi. (Wanawaambia): "Kama mkitolewa, (mkifukuzwa hapa) tutaondoka pamoja nanyi, wala hatutamtii yoyote kabisa juu yenu. Na kama mkipigwa vita lazima tutakusaidieni." Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia ya kuwa wao ni waongo.

12. Kama wakifukuzwa hawatatoka pamoja nao, na kama wakipigwa hawatawasaidia; na kama wakiwasaidia kwa yakini watageuza migongo (wende mbio); kisha hawatanusuriwa.

13. Hakika nyinyi (Waislamu) mnaogopwa zaidi katika nyoyo zao kuliko wanavyomuogopa Mwenyezi Mungu; maana wao ni watu wasiofahamu (lolote).

14. Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipokuwa katika vijiji vyao vilivyohifadhiwa, au nyuma ya kuta. Vita vyao baina yao vikubwa. Utawadhani kuwa wako pamoja; kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

15. Hali yao (hawa Mayahudi wa Kibanu Nadhir) ni kama ya wale (Mayahudi wa Bani Qaynuqai) waliowatangulia (kufikwa na baa) hivi karibuni; walionja ubaya wa mambo yao; na watapata adhabu (nyingine) iumizayo (vile vile).

16. Ni kama Shetani anapomwambia mtu: "Kufuru;" na anapokufuru akamwambia: "Mimi si pamoja nawe, hakika namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu."

17. Basi mwisho wa wote wawili hao ukawa

رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ
الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ
لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا
وَإِن قُوتِلْتُمْ لَنَنصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ
لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾

لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِن قُوتِلُوا لَا
يَنصُرُونَهُمْ وَلَئِن نَّصَرُوهُمْ لَيُوَلُّنَّ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا
يُنصَرُونَ ﴿١٢﴾

لَأَنتُمْ أَشَدُّ رَهْبَةً فِي صُدُورِهِم مِّنَ اللَّهِ
ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُونَ ﴿١٣﴾

لَا يُقَاتِلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرًى مُّحَصَّنَةٍ أَوْ مِن
وَرَاءِ جُدُرٍ بَأْسُهُم بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا
وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾

كَمَثَلِ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ
وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٥﴾

كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ
قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِّنكَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾

فَكَانَ عَاقِبَتَهُمَا أَنَّهُمَا فِي النَّارِ خَالِدَيْنِ فِيهَا

---

juu ya Waislamu wenzi wao. Basi natuwe namna hii ili tuwe pamoja na hao Muhajiri na Ansari katika kundi la Mwenyewe Mtume:

| | |
|---|---|
| Ya Rabi tuweke | Makazi mema |
| Ututimizie | Kila neema |
| Tupe Ridhwani | Tupe Rehema |
| Tuwe na Mtume | Katika Janna. |
| Na Jamaa zake | Wale Kiramu |
| Na Sahaba zake | Wote Idhamu |
| Na Matabiina | Na Maimamu |
| Na walio wetu | Kila namna. |

11-17. Visa vya Wanafiki wa Madina na Makafiri wa hapo na yaliyowafika mwisho wake. Hatapanda mtu miba akavuna zabibu.

ع وَذٰلِكَ جَزٰٓؤُا الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٧﴾

waingie Motoni kukaa humo daima; na hiyo ndiyo jaza ya madhalimu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ۗ اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٨﴾

18. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu; na kila mtu aangalie, (atazame) anayoyatanguliza kwa ajili ya kesho (Akhera); na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda (yote).

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ نَسُوا اللّٰهَ فَاَنْسٰىهُمْ اَنْفُسَهُمْ ۗ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿١٩﴾

19. Wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na (Mwenyezi Mungu) Akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio maasi wakubwa.

لَا يَسْتَوِيْٓ اَصْحٰبُ النَّارِ وَاَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ۗ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَآئِزُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi; watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.

لَوْ اَنْزَلْنَا هٰذَا الْقُرْاٰنَ عَلٰى جَبَلٍ لَّرَاَيْتَهٗ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللّٰهِ ۗ وَتِلْكَ الْاَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُوْنَ ﴿٢١﴾

21. Lau kama tungaliiteremsha hii Qurani juu ya mlima, ungaliuona ukinyenyekea (na) kupasuka kwa sababu ya hofu ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mifano tunawapigia (tunawaeleza) watu ili wafikiri.

هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۚ هُوَ الرَّحْمٰنُ الرَّحِيْمُ ﴿٢٢﴾

22. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu. Anayeyajuwa yaliyofichikana na yaliyo dhahiri. Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ اَلْمَلِكُ الْقُدُّوْسُ السَّلٰمُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيْزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۗ سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٢٣﴾

23. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu; Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye shani, Anayefanya analolitaka, Mkubwa. Mwenyezi Mungu Yu mbali na hao wanaomshirikisha naye.

هُوَ اللّٰهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى ۚ يُسَبِّحُ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٤﴾ ع

24. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mfanyaji wa sura (za namna namna za viumbe); Mwenye majina (sifa) mazuri. Kinamtukuza kila kilichomo mbinguni na ardhini. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

---

18. Tunahimizwa kuitengenezea Kesho yetu tusije tukasema *Yaa Laytany qaddamtu Lihayaty,* kama ilivyo katika Aya ya 24 ya *Suratul Fajr.* Konde ya kupandia utakayoyavuna Akhera iko hapa. *Addun-yaa Mazraatul Aakhira.*

19,20. Tusisahau kujitengezea au hatutakuwa sawa na hao watu wema. Watu wema ndio watakakuwa katika neema, na hao wengine watakuwa katika nakama (Naqma).

21. Kuonyesha moyo mgumu wa binadamu. Haulainiki hata kwa maneno ya Mwenyezi Mungu.

22-24. Aya hizi ni kama zile za mwanzo wa *Suratul Hadyd* kama tulivyotaja katika maelezo ya Aya za 1-6 za *Suratul Hadyd.*

آياتها ١٣ (٦٠) سورة الممتحنة مدنية (٩١) ركوعاتها ٢

Ina Aya 13 **SURATUL MUMTAHINAH** Ina Makara 2

*(Imeteremka Madina)*

بسم الله الرحمن الرحيم

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يا أيها الذين آمنوا لا تتخذوا عدوي وعدوكم
أولياء تلقون إليهم بالمودة وقد كفروا بما
جاءكم من الحق يخرجون الرسول وإياكم
أن تؤمنوا بالله ربكم إن كنتم خرجتم جهادا في
سبيلي وابتغاء مرضاتي تسرون إليهم بالمودة
وأنا أعلم بما أخفيتم وما أعلنتم ومن يفعله
منكم فقد ضل سواء السبيل ①

1\. Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki; mnaowapelekea (habari zenu) kwa ajili ya urafiki, hali ya kuwa wamekwishaikanusha haki iliyokujieni; wakamfukuza Mtume na nyinyi pia; kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola wenu, (pasina baya lolote mlilowafanyia). Mnapoondoka kufanya jihadi katika njia yangu na kuitafuta radhi yangu mnawapa siri (zenu za vita) kwa ajili ya mapenzi (yenu)! (Msifanye tena). Nami najua sana mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha. Na anayefanya hayo miongoni mwenu, basi amekwishaitupa njia iliyo sawa.

إن يثقفوكم يكونوا لكم أعداء ويبسطوا
إليكم أيديهم وألسنتهم بالسوء وودوا لو
تكفرون ②

2\. Wakikutana na nyinyi (katika midani za vita) wanakuwa maadui zenu; na wanakukunjulieni mikono yao (kukudhuruni) na ndimi zao kwa uovu. Na wanapenda muwe makafiri. (Bure nyinyi mnawapenda!).

لن تنفعكم أرحامكم ولا أولادكم يوم القيامة
يفصل بينكم والله بما تعملون بصير ③

3\. Hawatakufaeni jamaa zenu wala watoto wenu siku ya Kiama; Atapambanua (Mwenyezi Mungu) baina yenu, na Mwenyezi Mungu anaona yote mnayoyatenda.

قد كانت لكم أسوة حسنة في إبراهيم
والذين معه إذ قالوا لقومهم إنا برآء
منكم ومما تعبدون من دون الله كفرنا
بكم وبدا بيننا وبينكم العداوة والبغضاء
أبدا حتى تؤمنوا بالله وحده إلا قول إبراهيم
لأبيه لأستغفرن لك وما أملك لك من الله

4\. Hakika nyinyi muna mfano mzuri kwa (Nabii) Ibrahimu na wale waliokuwa pamoja naye; walipowaambia jamaa zao (makafiri): "Kwa yakini sisi tu mbali nanyi, na mbali na hayo mnayoyaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu (tumejiepusha na nyinyi na haya mnayoyaabudu); tunakukataeni, umekwishadhihiri uadui na bughudha ya daima baina yetu na nyinyi mpaka mtakapomuamini Mwenyezi Mungu peke yake." (Basi na nyie fanyeni hivi: muwakate jamaa zenu wa kikafiri, mumuige Nabii Ibrahimu) ila katika usemi wake Ibrahimu kumwambia baba yake: "Hakika nitakuombea msamaha, wala sina uweza wa chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu (ila huu tu." Basi msiige neno lake hili la kuwaombea dua makafiri,

---

4\. Tunaambiwa tuuwige mwendo wa Baba wa Sharia — Nabii Ibrahimu — na wafuasi wake; namna walivyojiepusha na wazee wao na jamaa zao waloikataa haki; wakawapiga vita barabara.

bali ombeni hivi): "Mola wetu! Tumetegemea kwako, na tumegeuka kuja kwako, na kwako tu ndiko marejeo (ya viumbe wote)."

مِنْ شَيْءٍ ۚ رَبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا وَإِلَيْكَ أَنَبْنَا
وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴿٤﴾

5. "Mola wetu! Usitufanye mtihani kwa wale waliokufuru, na tughufirie Mola wetu! Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima."

رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلَّذِينَ كَفَرُوا وَاغْفِرْ لَنَا
رَبَّنَا ۚ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٥﴾

6. Kwa yakini umekuwa mfano mzuri kwenu katika mwendo wao, kwa amuogopaye Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Na anayeyapuuza haya Mwenyezi Mungu ni Mkwasi Mwenye kusifiwa, (hamhitajii).

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيهِمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَنْ كَانَ يَرْجُوا
اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ
هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٦﴾

7. Asaa Mwenyezi Mungu atatia mapenzi baina yenu na hao maadui zenu, na Mwenyezi Mungu ni Muweza. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu; (atawawafikia kusilimu).

عَسَى اللَّهُ أَنْ يَجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ الَّذِينَ عَادَيْتُمْ
مِّنْهُمْ مَّوَدَّةً ۚ وَاللَّهُ قَدِيرٌ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾

8. Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia ihsani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakukufukuzeni katika nchi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu.

لَا يَنْهٰكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي
الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبَرُّوهُمْ
وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٨﴾

9. Mwenyezi Mungu anakukatazeni na wale ambao wanapigana nanyi katika dini, na kukufukuzeni katika nchi zenu, na wanasaidia katika kufukuzwa kwenu; (anakukatazeni) kuwafanya marafiki na wawafanyao marafiki basi hao ndio madhalimu.

إِنَّمَا يَنْهٰكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قٰتَلُوكُمْ فِي
الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظٰهَرُوا عَلَىٰ
إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولٰئِكَ
هُمُ الظّٰلِمُونَ ﴿٩﴾

10. Enyi mlioamini! Watapokujieni wanawake Waislamu wanaohama, basi wafanyieni mtihani — na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi imani yao. Mkiona kuwa wao ni Waislamu kweli basi msiwarudishe (kwao Makka) kwa makafiri. (Wanawake) hawa si halali kwa hao (wanaume makafiri), wala wao (wanaume makafiri) si halali kwao; na warudishieni (waume zao) mali zao, (mahari) walizotoa. Wala kwenu si hatia kuwaoa,

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوٓا إِذَا جَآءَكُمُ الْمُؤْمِنٰتُ
مُهٰجِرٰتٍ فَامْتَحِنُوهُنَّ ۚ اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمٰنِهِنَّ ۚ فَإِنْ
عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنٰتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ ۚ
لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ ۚ وَآتُوهُمْ
مَّآ أَنْفَقُوا ۚ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ إِذَا

---

5. "Usitufanye mtihani kwa wale waliokufuru," dhahiri yake ina tafsiri mbili. Usitufanye kuonewa na makafiri. (a) Tukataabika sisi au (b) Wao makafiri wakazidi kuukataa Uislamu kwa kuwa si dini ya haki hiyo, kwani ingekuwa dini ya haki wasingetaabishwa watu wake.

7. Wala wasione vibaya kukatana hivyo na jamaa zao kwani hao jamaa zao walio katika batili — wakiona wametupwa hivyo na hao jamaa zao waliomo katika haki — watakuja katika haki, wawe mkono mmoja katika kheri, si mkono mmoja katika batili.

8,9. Na Mwenyezi Mungu hatukatazi kuwafanyia makafiri wema na insafu. Bali anatuamrisha tuwafanyie haya.

ikiwa mtawapa mahari yao. Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu. na takeni (kwa watakaowaoa) mahari mliyoyatoa; nao (makafiri wanaume) nawatake mahari waliyotoa (kwa wanaume watakaowaoa wake zao waliosilimu wakakimbilia Madina). Basi hii ndiyo hukumu ya Mwenyezi Mungu anayokuhukumuni; na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi, Mwenye hikima.

آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۚ وَلَا تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ
وَاسْأَلُوا مَا أَنفَقْتُمْ وَلْيَسْأَلُوا مَا أَنفَقُوا ۚ ذَٰلِكُمْ
حُكْمُ اللَّهِ ۖ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ ۚ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾

11. Na kama akitoroka yoyote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, tena ikatokea bahati (ya kupata nyinyi Waislamu ngawira) basi wapeni wale ambao wake zao wametoroka, kiasi cha mahari waliyotoa, na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.

وَإِن فَاتَكُمْ شَيْءٌ مِّنْ أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ
فَعَاقَبْتُمْ فَآتُوا الَّذِينَ ذَهَبَتْ أَزْوَاجُهُم مِّثْلَ
مَا أَنفَقُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنتُم بِهِ
مُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

12. Ewe Nabii! Watakapokujia wanawake walioamini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na cho chote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawaua watoto wao, wala hawataleta uzushi wanaouzusha tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi peana ahadi nao na uwatakie maghufira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa rehema.

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعْنَكَ عَلَىٰ
أَن لَّا يُشْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا
يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ
يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ وَلَا يَعْصِينَكَ فِي
مَعْرُوفٍ ۙ فَبَايِعْهُنَّ وَاسْتَغْفِرْ لَهُنَّ اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ
غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

13. Enyi mlioamini! Msifanye urafiki wa ndani na watu ambao Mwenyezi Mungu amewakasirikia; na wamekata tamaa ya (kupata thawabu za) Akhera (kwani wanajijua vizuri kuwa wanafanya mabaya) kama walivyokwishakata tamaa makafiri waliokwishazikwa.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ
قَدْ يَئِسُوا مِنَ الْآخِرَةِ كَمَا يَئِسَ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ
الْقُبُورِ ﴿١٣﴾

---

10. Tazama uadilifu wa Uislamu. Kuwa wakija Madina wanawake wa kikafiri wanatoka Makka, na waume zao wako Makka, wakamwambia Mtume kuwa wamesilimu, basi asiwapokee tu Mtume; bali awafanyie mtihani barabara mpaka umdhihirikie Uislamu wao ndipo awachukue; na akiwachukua awapelekee mahari yao waume zao makafiri — awapelekee fedha walizowaolea. Kuna insafu zaidi kuliko hii? Na Mtume aliwafanyia. Na mmoja katika wanawake hao ni Bibi Ummu Kulthum binti Uqba bin Aby Muayt — baba yake alikuwa kafiri mwenye chuki kubwa kabisa juu ya Mtume na Waislamu wote.

Na makafiri wakaambiwa nao wakiwaoa wake wa Waislamu — walioko ukafirini huko — walete mahari yao. Lakini hawakukubali. Basi Mtume akawa anawalipa Waislamu hawa — walionyimwa haki ya mahari yao — alikuwa anawalipa katika pesa zinazopatikana katika ngawira (nyara), kama ilivyo katika Aya 11 hapa. Wala hakuwalipizia kisasi makafiri kuwa na sisi hatutakuleteeni mahari ya wake zenu waliokuja kwetu, maadamu nyinyi mnakataa kutoa. Hapana kulipa mabaya. Mmoja katika hao wanawake waliomili ukafirini ni mke wa Sayyidna Umar bin Al Khattab — Qureyba binti Aby Umayya, mtoto wa shangazi lake Mtume ndugu wa kuumeni wa mkewe Mtume, Bibi Hind binti Aby Umayya. Katika wanawake waliokuwa wazuri sana wa sura. Mwisho alirejea Uislamuni, akaolewa na Sayyidna Muawiya.

12. Baadhi ya ahadi hizi walizokuwa wakipewa wanawake, walikuwa wakipewa wanaume vile vile, kabla ya hapa na baada yake.

13. Wakubwa wa Kiyahudi walikuwa na yakini kuwa wataingia Motoni tu kwani walikuwa wana yakini kuwa wanakwenda kinyume na Mtume kwa inda tu.

اٰيَاتُهَا ١٤ (٦١) سُوْرَةُ الصَّفِّ مَدَنِيَّةٌ (١٠٩) رُكُوْعَاتُهَا ٢

*Ina Aya 14* **SURATUS SAFF** *Ina Makara 2*

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

سَبَّحَ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ (١)

2. Enyi mlioamini! Mbona, (kwa nini) mnasema msiyoyatenda?

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لِمَ تَقُوْلُوْنَ مَا لَا تَفْعَلُوْنَ (٢)

3. Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda.

كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللّٰهِ اَنْ تَقُوْلُوْا مَا لَا تَفْعَلُوْنَ (٣)

4. Kwa yakini Mwenyezi Mungu anawapenda wale wanaopigana katika njia yake, safusafu, (mkono mmoja); kama kwamba wao ni jengo lililokamatana bara bara.

اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الَّذِيْنَ يُقَاتِلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِهٖ صَفًّا كَاَنَّهُمْ بُنْيَانٌ مَّرْصُوْصٌ (٤)

5. Na wakumbushe, (Nabii) Musa alipowaambia watu wake: "Enyi watu wangu! Mbona, (kwa nini) mnaniudhi, hali mnajua kuwa mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (niliyeletwa) kwenu?" Basi walipoendelea na uovu wao, Mwenyezi Mungu aliziachilia nyoyo zao zipotoke (kama walivyotaka wenyewe); na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu waovu (wenye kutoka katika taa yake).

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ يٰقَوْمِ لِمَ تُؤْذُوْنَنِيْ وَقَدْ تَّعْلَمُوْنَ اَنِّيْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ ؕ فَلَمَّا زَاغُوْۤا اَزَاغَ اللّٰهُ قُلُوْبَهُمْ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ (٥)

6. Na (wakumbushe) aliposema (Nabii) Isa bin Mariamu (kuwaambia Mayahudi): "Enyi wana wa Israili! Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na kutoa habari njema ya Mtume atakayejia nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. (Muhammad. Na maana ya majina mawili yote haya ni moja. Maana yake Mwenye kushukuriwa kwa maneno yake mazuri na vitendo vyake vizuri na kila chake kwani vyake vyote ni vizuri). Lakini alipowajia kwa hoja zilizo wazi, walisema: "Huu ni udanganyifu uliyo dhahiri."

وَاِذْ قَالَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ يٰبَنِيْۤ اِسْرَآءِيْلَ اِنِّيْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرٰىةِ وَمُبَشِّرًۢا بِرَسُوْلٍ يَّاْتِيْ مِنْۢ بَعْدِي اسْمُهٗۤ اَحْمَدُ ؕ فَلَمَّا جَآءَهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ قَالُوْا هٰذَا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ (٦)

---

2,3. Katika mambo yanayomuudhi Mwenyezi Mungu kweli kweli ni kuwa mtu maneno yake mazuri, na vitendo vyake ni vibaya — anadanganya watu.

4. Mwenyezi Mungu anataka Waislamu wote wawe mkono mmoja katika kuuendesha Uislamu mbele.

7. Na ni nani dhalimu mkubwa wa nafsi yake kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, na hali anaitwa katika Uislamu? Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu (wa nafsi zao).

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعَىٰ إِلَى الْإِسْلَامِ ۚ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٧﴾

8. Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukiwa.

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٨﴾

9. Yeye ndiye aliyemtuma (aliyemleta) Mtume wake (Nabii Muhammad) kwa uwongofu na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa washirikina watachukiwa.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

10. Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo?

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ تِجَارَةٍ تُنْجِيكُمْ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾

11. (Basi biashara yenyewe ni hii): Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua (kuwa ni bora, basi fanyeni)

تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

12. (Mkifanya haya) Atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika Mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele: huku ndiko kufuzu kukubwa

يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسَاكِنَ طَيِّبَةً فِي جَنَّاتِ عَدْنٍ ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾

13. Na (atakupeni) kingine mnachokipenda: Nayo ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu na ushindi ulio karibu! Na wapashe habari njema Waislamu.

وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا ۖ نَصْرٌ مِنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾

14. Enyi mlioamini! Kuweni wasaidizi wa (kutangaza dini ya) Mwenyezi Mungu, kama alivyosema Isa bin Mariamu kuwambia wafuasi (wake maneno haya): "Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya (kutangaza dini ya) Mwenyezi Mungu?" Wafuwasi wakasema: "Sisi ni wasadizi wa (kutangaza dini ya) Mwenyezi Mungu." Basi taifa moja la wana wa Israili liliamini, na taifa jingine lilikufuru; basi tukawatia nguvu wale walioamini juu ya maadui zao na wakawa wenye kushinda.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا أَنْصَارَ اللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ لِلْحَوَارِيِّينَ مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ ۖ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ۖ فَآمَنَتْ طَائِفَةٌ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَتْ طَائِفَةٌ ۖ فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ آمَنُوا عَلَىٰ عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ ﴿١٤﴾

---

8,9. Mwenyezi Mungu anabashiri kuwa Uislamu utakwenda mbele tu hata wakipania vipi makafiri kuupinga. Makadiyani Katika Aya waliyifanya ya 10 wametia ukafiri wa kumdaia Unabii Isa huyo mtu wao, na kusema ametajwa na Mtume kwa jina la Masihi aliyeahidiwa. Tumebainisha katika Aya ya 115 ya *Suratul Baqarah* uwongo na ukafiri huu, na katika Aya nyengine. Sasa huko kumtaja kwao Ibni Jarir na Razy ni kutaka kuzua tu na kupoteza Waislamu.

11-14. Yanatajwa mambo mazuri kabisa ya kufanya, na nini tunza (tuzo) yake. Basi cheza mchezo huu wa kheri apate Mola wako kukutunza (kukutuza).

اياتها ١١ (٦٢) سورة الجمعة مدنية (١١٠) ركوعاتها ٢

*Ina Aya 11* *Ina Makara 2*

# SURATUL JUMUA

*(Imeieremka Madina)*

بسم الله الرحمن الرحيم

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يسبح لله ما في السموت وما في الارض الملك
القدوس العزيز الحكيم ①

1. Vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi vinamtukuza Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

هو الذي بعث في الاميين رسولا منهم يتلوا عليهم
ايته ويزكيهم ويعلمهم الكتب والحكمة وان
كانوا من قبل لفي ضلل مبين ②

2. Yeye ndiye aliyeleta Mtume katika watu wasiojua kusoma, anayetokana na wao, awasomee Aya zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hikima, (ilimu nyinginezo). Na kabla ya haya walikuwa katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri

واخرين منهم لما يلحقوا بهم وهو العزيز
الحكيم ③

3. Na (amemleta) kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. (Nao ndio sisi Waislamu tuliokuja nyuma). Na yeye (Mwenyezi Mungu) ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

---

2-4. Tunatajiwa fadhila za kuletwa Nabii Muhammad (s.a.w.). Basi *Alhamdu Lillahi — Iladhy Hadaana Lihaadha Wamaa Kunnaa Linahtadiya Lawlaa Anhadaanallah.*

3. Makadayani Katika Aya hii waliyoifanya ya 4 wametia ukafiri wa kugeuza maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtumewe ili wampachikie Utume mtu wao. Mara yeye (a) Mtume tu, mara yeye (b) Ndiye Nabii Isa, mara (c) yeye ndiye Mahdi, mara (d) yeye Khalifa. Na ukafiri wote huo tumekwisha kuujibu. Sasa wanasema yeye ni Muajemi kama Salmanul Farsy.

Aya hii kama tunavyoiona — na kama wanavyoiona — inataja Uma wa watu wasiokuwa Waarabu watakaofuata Uislamu baada ya kufuata hao Waarabu; na Mtume amesema kuwa Mafursi (Maajemi) watakuwa wa mbele katika jambo hili la kufuata Uislamu; hakusema katika kupata Utume. Basi Mafursi wote wangekuwa Mitume! Ama wazandiki kweli kweli. Hawamuogopi Mwenyezi Mungu chembe, katika kutaka kupoteza Waislamu. Ama kani yao kubwa kabisa katika kutaka kuwapoteza Waislamu. Hata mwenye *Ruuhul Maany* — tafsiri wanayojidai kuitegemea — katika sahifa 83 ya Juzuu 28 ameitaja Hadithi hiyo ya Mtume kwa wingi, (Jam-u = plural) kuwa Mtume amesema: "Hata Uislamu ungekuwa uko katika nyota ya THUREYYA, wangeupata watu hawa wa Kifursi." Akasema kuwa hivi ndivyo Al-Bukhari, Attirmidhi, Annasai na wengineo wote walivyopokea. Na vivi hivi ndivyo Imam Ash Shawkany katika Sahifa 220 ya Juzuu ya 5 ya tafsiri yake anayoifasiri kwa Hadithi za Mtume, inayoitwa Fat-hul Qadir alivyoitaja Hadithi hii kwa wingi: "*Rijaalun Min Abnaai Faris*" (= Watu katika Maajemi). Hakusema "*Rajulun*"— Mtu mmoja tu. Akasema kuwa hivi ndivyo alivyopokea Al-Bukhari, Muslim, Said bin Mansur na Ibni Mardawayhi. Wao wametaja upokezi wa mtu mmoja ili awe huyo mtu wao. Mafursi wangapi wanavyoni wakubwa wa Kiislamu wasiokuwa na mfano, kwa nini wasiwe wao, awe yeye anaejipa sasa Ufursi? Maimamu wa ilmu zote za Kiislamu walikuwa hao Mafursi aliowataja Mtume; wala hapana mmoja katika hao aliyejidai Utume. Nitamtaja Imam mmoja tu katika kila namna moja ya ilimu katika ilimu za Kiislamu:

Katika Ilimu ya Kuisoma Qurani, Ibni Kathyr; katika ilimu ya Kuifasiri Qurani, Ibni Jaryr; katika Ilimu ya Hadithi, Al Bukhary; katika Ilimu ya Tarikhi ya Mtume, Ibni Is-haq; katika Ilimu ya Tarikhi ya Kiarabu, Abu Ubeyda; katika Ilimu ya Fiqh, Abu Hanyfa; katika Ilimu ya Lugha ya Kiarabu, Al Fayruuzabaadhy; katika Ilimu ya Nahw, Sybawayhi; katika Ilimu ya Sarf, Al Kisai; katika Ilimu ya Tasawwuf, Al Hasan Al Bisry; katika Ilimu

4. Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu anayompa amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.

ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ ذُو
الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ④

5. Mfano wa wale waliopewa Taurati, kisha hawakuichukua (kwa kuitumia) ni kama punda anayebeba vitabu vikubwa vikubwa (bila kupata nafuu kwavyo). Ni m-baya kabisa mfano wa watu waliozikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu.

مَثَلُ الَّذِينَ حُمِّلُوا التَّوْرَاةَ ثُمَّ لَمْ يَحْمِلُوهَا كَمَثَلِ
الْحِمَارِ يَحْمِلُ أَسْفَارًا ۚ بِئْسَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ
كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ ۚ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ
الظَّالِمِينَ ⑤

6. Sema: "Enyi Mayahudi! Kama mnadai ya kuwa nyinyi ni wapenzi wa Mwenyezi Mungu pasipokuwa watu wengine, basi yatamanini mauti (mwendezenu Peponi kwa Mwenyezi Mungu), ikiwa mnasema kweli."

قُلْ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ هَادُوا إِن زَعَمْتُمْ أَنَّكُمْ أَوْلِيَاءُ
لِلَّهِ مِن دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوُا الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ
صَادِقِينَ ⑥

7. Lakini hawatayatamani kabisa kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao; na Mwenyezi Mungu anawajua madhalimu.

وَلَا يَتَمَنَّوْنَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ۚ وَاللَّهُ
عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ⑦

8. Sema: "Hakika mauti haya mnayoyakimbia, bila shaka yatakutana nanyi; kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; hapo atakujulisheni (yote) mliyokuwa mkiyatenda."

قُلْ إِنَّ الْمَوْتَ الَّذِي تَفِرُّونَ مِنْهُ فَإِنَّهُ مُلَاقِيكُمْ ۖ
ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم
بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ⑧ ع

9. Enyi mlioamini! Kukiadhiniwa kwa ajili ya Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kumtaja Mwenyezi Mungu na acheni biashara. Kufanya hivi ni bora kwenu. Ikiwa mnajua (hivi basi fanyeni).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِن يَوْمِ
الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ۚ ذَٰلِكُمْ
خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ⑨

10. Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi (ili msipate kufanya mabaya), ili mpate kufaulu.

فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِن
فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ⑩

---

ya Khati ya Kiarabu, Ibn Muqlah; katika Ilimu ya Kufundisha kuandika kwa ufasihi wa Kiarabu, Abdul Qadiri Jurjany; katika Ilimu ya Kufundisha kutunga mashairi ya Kiarabu, Al Farraa. Katika Kuandika kwa ufasihi kwa mashairi ya Kiarabu, At Tughrai; katika Kuandika kwa ufasihi kwa Kiarabu si kwa mashairi, Ibnul Muqaffaa; katika Kusema kwa ufasihi kwa lugha ya Kiarabu, Wasil; katika kuandika hadithi kwa lugha ya Kiarabu, Al Jaahidh.

Na wengi mno kabisa kuliko hawa. Wala hakuna mmoja aliyedai Utume au aliyedaiwa Utume.

5. Unatajwa ubaya wa kutofuata kheri unayoijua.

9. Makadiyani Katika Aya waliyoifanya ya 10 wameingilia madhehebu. Wala haiwakhusu kitu kuingia madhehebu ya watu; wala Mtume hakutaja idadi ya watu wa kusali Ijumaa. Bali kila Imamu wa madhehebu alijitahidi mwenyewe kwa ilimu yake na jitihada yake. Haiwakhusu kitu wao.

9,10. Siku ya Ijumaa haikatazwi kufanya kazi, kinyume cha wanavyodhani baadhi ya watu. Wanaambiwa ukifika wakati wa kusali wende wakasali — sio wasifanye kazi kutwa. Na ikisha Sala watoke wakafanye kazi zao kama walivyokuwa wakifanya. Mayahudi ndio waliopewa mtihani wa kutofanya kazi Jumamosi. Waislamu hawakupewa amri hiyo wala hawakusunishiwa.

11. Na wanapoiona biashara au mchezo wanavikimbilia hivyo, wakakuacha umesimama (peke yako unakhutubu pamoja na watu wachache kabisa wasiofuatia hayo). Sema: "Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mchezo na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoa riziki."

وَإِذَا رَأَوْا تِجَارَةً أَوْ لَهْوًا انْفَضُّوا إِلَيْهَا وَ
تَرَكُوكَ قَائِمًا ۚ قُلْ مَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ مِنَ
اللَّهْوِ وَمِنَ التِّجَارَةِ ۚ وَاللَّهُ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿١١﴾

---

11. Walifanya makosa siku moja — wakatoka baadhi yao, na Mtume anakhutubu. Basi wanalaumiwa hivi. Haifai mtu kuondoka katika jambo la kheri ila kwa dharura kubwa. Na wao hawakuwa na dharura hiyo wakati huo.

اٰيَاتُهَا ١١ (٦٣) سُوْرَةُ الْمُنٰفِقُوْنَ مَدَنِيَّةٌ (١٠٤) رُكُوْعَاتُهَا ٢

*Ina Aya 11* **SURATUL MUNAAFIQUN** *Ina Makara 2*

*(Imeteremka Madina)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.**

إِذَا جَآءَكَ الْمُنٰفِقُوْنَ قَالُوْا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُوْلُ اللّٰهِ ۘ
وَاللّٰهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُوْلُهٗ ؕ وَاللّٰهُ يَشْهَدُ إِنَّ
الْمُنٰفِقِيْنَ لَكٰذِبُوْنَ ۚ ﴿١﴾

**1. Wanapokujia wanafiki, husema: "Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu." Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wake na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo, (wanasema wasiyoyasadiki).**

اِتَّخَذُوْٓا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ
اللّٰهِ ؕ إِنَّهُمْ سَآءَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٢﴾

**2. Wamevifanya viapo vyao ndizo ngao za kujikingia, wakajikinga na kupitishwa njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakifanya.**

ذٰلِكَ بِأَنَّهُمْ اٰمَنُوْا ثُمَّ كَفَرُوْا فَطُبِعَ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَهُمْ
لَا يَفْقَهُوْنَ ﴿٣﴾

**3. Na hayo ni kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo muhuri umepigwa juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawafahamu lolote.**

وَإِذَا رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ ؕ وَإِنْ يَّقُوْلُوْا
تَسْمَعْ لِقَوْلِهِمْ ؕ كَأَنَّهُمْ خُشُبٌ مُّسَنَّدَةٌ ؕ يَحْسَبُوْنَ
كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ؕ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ ؕ
قٰتَلَهُمُ اللّٰهُ ۫ أَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ﴿٤﴾

**4. Na unapowaona, miili yao inakupendeza, na kama wakisema, unasikiliza usemi wao (kwa vile unavyopendeza); lakini wao ni kama boriti zilizotegemezwa; (wamekaa magogo tu hapo, hawafahamu lolote); wanadhani kila kishindo (kinachozuka) ni juu yao, (ni cha kuwatafuta wao). Hao ni maadui, jihadhari nao. Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki!**

وَإِذَا قِيْلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُوْلُ
اللّٰهِ لَوَّوْا رُءُوْسَهُمْ وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّوْنَ وَهُمْ
مُّسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٥﴾

**5. Na wanapoambiwa: "Njooni ili Mtume wa Mwenyezi Mungu akuombeeni msamaha (kwa makosa yenu mliyoyafanya)," huvigeuza vichwa vyao (kwa kuonyesha kuwa hawataki); na unawaona wanajizuia na wakijiona wakubwa.**

سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ
لَهُمْ ؕ لَنْ يَّغْفِرَ اللّٰهُ لَهُمْ ؕ إِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِي
الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ ﴿٦﴾

**6. Ni sawa kwao ukiwatakia msamaha au usiwatakie msamaha, Mwenyezi Mungu hatawasamehe; hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu maasi (wenye kutoka katika taa yake).**

---

1. Sura hii inataja baadhi kidogo ya habari za wanafiki na baadhi ya mambo waliyokuwa wakimfanyia Mtume na Masahaba.

7. Hao ndio wanaosema: "Msitoe mali kwa ajili ya wale walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ili waondokelee mbali (hapa nchini kwetu, Madina)." Na hazina za mbingu na ardhi ni za Mwenyezi Mungu; lakini wanafiki hawafahamu.

هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنْفِقُوا عَلَىٰ مَنْ عِنْدَ
رَسُولِ اللَّهِ حَتَّىٰ يَنْفَضُّوا ۗ وَلِلَّهِ خَزَائِنُ
السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ ۝٧

8. Wanasema: "Tukirudi Madina, Mwenye utukufu atamfukuza mnyonge," (yaani hilo kubwa lao la unafiki linaloitwa Abdalla bin Ubay litamtoa Mtume). Na utukufu hasa ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wa Waislamu; lakini wanafiki hawajui.

يَقُولُونَ لَئِنْ رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لَيُخْرِجَنَّ
الْأَعَزُّ مِنْهَا الْأَذَلَّ ۚ وَلِلَّهِ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ
وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَٰكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۝٨ ع

9. Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu wala watoto wenu kumkumbuka Mwenyezi Mungu; Na wafanyao hayo, hao ndio wenye kuhasirika.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُلْهِكُمْ أَمْوَالُكُمْ وَلَا
أَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ۚ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَٰلِكَ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ۝٩

10. Na toeni katika yale tuliyokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti, kisha akasema: "Mola wangu! Huniakhirishi muda kidogo (tu) nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watendao mema?"

وَأَنْفِقُوا مِنْ مَا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ
أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ
أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُنْ مِنَ الصَّالِحِينَ ۝١٠

11. Lakini Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapokuja ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda (yote).

وَلَنْ يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجَلُهَا ۚ وَاللَّهُ خَبِيرٌ
بِمَا تَعْمَلُونَ ۝١١ ع

---

9,10. Walicho nacho lazima watowe au watakuja kujuta wakati ambao kutubia kwao hakutawafaa kitu.

اٰيَاتُهَا ١٨ سُوْرَةُ التَّغَابُنِ مَدَنِيَّةٌ (١٠٨) (٦٤) رُكُوْعَاتُهَا ٢

*Ina Aya 18*

# SURATUT TAGHAABUN

*Ina Makara 2*

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Kinamtukuza Mwenyezi Mungu kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini; ufalme ni wake, na sifa njema ni zake, na yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

يُسَبِّحُ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ لَهُ
الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ۖ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ١

2. Yeye ndiye aliyekuumbeni (nyote). Na kuna wengine wenu ni makafiri na wengine wenu ni Waislamu. Na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyafanya.

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَّمِنْكُمْ مُّؤْمِنٌ ۚ
وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ٢

3. Ameumba mbingu na ardhi kwa haki; na akafanya sura zenu, kisha sura zenu (hizo) akazifanya nzuri. Na marejeo ni kwake.

خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ وَصَوَّرَكُمْ
فَاَحْسَنَ صُوَرَكُمْ ۚ وَاِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ٣

4. (Mwenyezi Mungu) anajua vilivyomo mbinguni na ardhini, na anajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani, (seuze yaliyo dhahiri).

يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا
تُسِرُّوْنَ وَمَا تُعْلِنُوْنَ ۚ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ بِذَاتِ
الصُّدُوْرِ ٤

5. Je! Haikukujieni habari ya wale waliokufuru zamani huko; na wakaonja ubaya wa mambo yao? Na wao wana adhabu iumizayo (mpaka sasa na mpaka Kiama).

اَلَمْ يَاْتِكُمْ نَبَؤُا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَبْلُ ۚ فَذَاقُوْا
وَبَالَ اَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ٥

6. Hayo ni kwa sababu Mitume wao walikuwa wakiwajia kwa hoja waziwazi; lakini wakisema: "Oh! Watu wenzetu ndio watuongoze?" Kwa hivyo walikanusha na wakageuka upande. Na Mwenyezi Mungu si muhitaji; bali Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, Mwenye kusifiwa.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُ كَانَتْ تَّاْتِيْهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ
فَقَالُوْا اَبَشَرٌ يَّهْدُوْنَنَا ۚ فَكَفَرُوْا وَتَوَلَّوْا
وَّاسْتَغْنَى اللّٰهُ ۚ وَاللّٰهُ غَنِيٌّ حَمِيْدٌ ٦

7. Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: "Kwa nini? Kwa haki ya Mola wangu nyinyi lazima mtafufuliwa; kisha lazima mtajulishwa mliyoyatenda (na mlipwe kwayo). Na hayo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu."

زَعَمَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا اَنْ لَّنْ يُّبْعَثُوْا ۚ قُلْ بَلٰى
وَرَبِّيْ لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذٰلِكَ
عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ٧

8. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na nuru tuliyoiteremsha, (Qurani). Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote.

فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَالنُّوْرِ الَّذِيْٓ اَنْزَلْنَا ۚ
وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ٨

9. (Kumbukeni) siku atakayokukusanyeni kwa ajili ya siku ya Makusanyiko (ya viumbe vyote). Hiyo ni siku ya hasara (kwa wabaya). Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu atamfutia maovu yake na atamwingiza katika mabustani (peponi) yapitayo mito mbele yake, wakae humo milele, huko ndiko kufaulu kukubwa.

يَوْمَ يَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ ذَٰلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ۗ
وَمَنْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُكَفِّرْ
عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ
الْعَظِيمُ ﴿٩﴾

10. Na wale waliokufuru na wakakadhibisha Aya zetu, hao ni watu wa Motoni, watakaa humo daima, nayo ni marejeo mabaya.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ
أَصْحَابُ النَّارِ خَالِدِينَ فِيهَا ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٠﴾

11. Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na anayemuamini Mwenyezi Mungu huuongoza moyo wake (kwendea maliwaza mazuri). Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ
يُؤْمِنْ بِاللَّهِ يَهْدِ قَلْبَهُ ۚ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾

12. Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume. Mkipuuza (hapana lawama juu yake). Juu ya Mtume wetu ni kufikisha tu kuliko waziwazi. (Naye amekwisha kukufikishieni).

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ ۚ فَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ
فَإِنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿١٢﴾

13. Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye tu. Na Waislamu wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ
الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٣﴾

14. Enyi mlioamini! Kwa yakini baadhi ya wake zenu na watoto wenu ni maadui zenu; basi jihadharini nao; na mkiwasamehe na kupuuza (yaliyopita) na kuyafuta (kabisa katika nyoyo zenu, basi Mwenyezi Mungu atafurahi) kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ وَ
أَوْلَادِكُمْ عَدُوًّا لَكُمْ فَاحْذَرُوهُمْ ۚ وَإِنْ تَعْفُوا
وَتَصْفَحُوا وَتَغْفِرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤﴾

15. Bila shaka mali zenu na watoto wenu ni jaribio (kwenu, mtihani kutazamwa mtakhalifu amri

إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ ۚ وَاللَّهُ

---

11. Wanazidi kuambiwa watu wasiitakidi marogo wala kama haya; wakati wanapofikwa na yanayowafika ikawa mbio kwa warogaji na warogowaji. Yasiwe haya. Mambo yote yamo katika Mkono wa Mwenyezi Mungu.

| | |
|---|---|
| Wakikushituwa | Wewe sishituke |
| Yupi awezaye | Kupitisha lake |
| Wakiwa na lao | Mungu ana yake. |
| Basi natutuwe nyoyo zetu | |
| Tabaradi | Nguvu za Mungu ni bora |
| Hazifidi | Nyingi za watu busara |
| Halirudi | Landikwalo na Qudura. |

Tushike haya yaliomo katika Aya ya 11 na ya 13 za Sura hii na ya namna hii na mengineyo yaliyomo katika Sura nyingine.

14,15. Inataka mtu ashike mizani barabara. Akipe kila kitu haki yake. Na mara nyingi — kwa ajili ya kupenda sana mtu mali — anavunganyiza haki za watu kwa ajili ya kuongeza mali yake. Na vile vile kwa ajili ya kupenda watoto wake, ndio ananyang'anya huku, akapokonya huko, akamegua hapa, akabwakuwa kule. Basi naogope kutawaliwa na mapenzi ya mali na watoto mpaka yakamfikisha au yakamsogeza katika daraja hii au chini kuliko daraja hii, seuze zaidi.

عِنْدَهٗٓ اَجْرٌ عَظِيْمٌ ﴿١٥﴾

za Mwenyezi Mungu kwa ajili yao au mtafuata amri zake). Na kwa Mwenyezi Mungu kuna ujira mkubwa kabisa.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَاسْمَعُوْا وَ اَطِيْعُوْا
وَاَنْفِقُوْا خَيْرًا لِّاَنْفُسِكُمْ ۗ وَمَنْ يُّوْقَ شُحَّ
نَفْسِهٖ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Mcheni Mwenyezi Mungu muwezavyo, (mwisho wa jitihada yenu). Na sikilizeni (mnayoambiwa) na tiini na toeni (katika njia za kheri); itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na wenye kuepushwa na ubakhili wa nafsi zao, hao ndio wenye kufaulu.

اِنْ تُقْرِضُوا اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا يُّضٰعِفْهُ لَكُمْ
وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللّٰهُ شَكُوْرٌ حَلِيْمٌ ﴿١٧﴾

17. Mkimkatia Mwenyezi Mungu sehemu nzuri (katika mali zenu, mkazitoa katika njia za kheri) atakuzidishieni na atakughufirieni. Na Mwenyezi Mungu ndiye atoaye thawabu nyingi, Mpole

عٰلِمُ الْغَيْبِ وَ الشَّهَادَةِ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿١٨﴾

18. Ajuaye siri na dhahiri, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

اٰيَاتُهَا ١٢ (٦٥) سُوْرَةُ الطَّلَاقِ مَدَنِيَّةٌ (٩٩) رُكُوْعَاتُهَا ٢

*Ina Aya 12* — *Ina Makara 2*

# SURATUT TALAQ

*(Imeteremka Madina)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يٰٓاَيُّهَا النَّبِيُّ اِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَآءَ فَطَلِّقُوْهُنَّ
لِعِدَّتِهِنَّ وَاَحْصُوا الْعِدَّةَ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ رَبَّكُمْ ۚ
لَا تُخْرِجُوْهُنَّ مِنْ بُيُوْتِهِنَّ وَلَا يَخْرُجْنَ
اِلَّآ اَنْ يَّاْتِيْنَ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ ۗ وَتِلْكَ
حُدُوْدُ اللّٰهِ ۗ وَمَنْ يَّتَعَدَّ حُدُوْدَ اللّٰهِ فَقَدْ
ظَلَمَ نَفْسَهٗ ۗ لَا تَدْرِيْ لَعَلَّ اللّٰهَ يُحْدِثُ
بَعْدَ ذٰلِكَ اَمْرًا ①

1. Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Mtakapotoa talaka kwa wanawake (mtakapowaacha) toeni talaka katika wakati wa eda zao. (Yaani waacheni wakati wa'tahara zao ambazo katika tahara hizo hamkuwahi bado kuwaingilia. Huna ruhusa kumuacha saa utakayo tu). Na fanyeni hisabu ya (siku za) eda, (zisije zikesha kabla hamjawarejea). Na Mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe. (Mwanamke akiwachwa asitoke katika nyumba hiyo; akae papo hapo kwa kulishwa na ku vi shwa mpaka eda ishe); Ila wakifanya jambo la ufasiki ulio wazi, (hapo ndio wanaweza kutolewa). Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anayeiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui (sababu ya kuamrishwa haya): labda Mwenyezi Mungu atatokezesha jambo jingine baada ya haya (yaani jambo la kupatana).

---

1. Sura hii inataja habari nyingi zilizokhusiana na Talaka. Na talaka kama alivyosema Mtume dhahiri shahiri katika Hadithi zake — na kama ilivyo katika dhahiri ya Qurani — ni Halali asiyoipenda Mwenyezi Mungu.

Imewekwa itokee itakapotokea dharura — iwe kama dawa, si chakula. Na wenye kuoana wa kikwetu wameifanya talaka ndicho chakula cha ndoa, lazima kutokea kwa kila mwenye kuoa.

Basi hapa zinatajwa kidogo sharti za kuacha:

(1) *Fatalliquuhunna Liiddatihinn:*

Na Mtume alifasiri tamko hili kwa kuwa hapana ruhusa kumwacha mwanamke anapokuwa yumo (a) Miezini au yumo (b) Katika Tahara, lakini wamepata kuonana katika Tahara hiyo.

Mwanamume akipandwa na hamaki akataka kumuacha mkewe hana ruhusa kumwambia: "Nimekuacha." Lazima amuulize kwanza yumo Miezini, (katika Hedhi) au Safi. Akiwa yumo Miezini hana ruhusa kumuacha. Akimuacha atapata dhambi. Wala mtu asiyaonee ajabu haya. Haya yanatajwa katika vitabu vyote vya Fiqhi, vikubwa na vidogo — hata katika kijitabu kidogo hiki cha Safina.

Kama yumo Miezini basi itampasa angojee mpaka aingie katika Tahara ndipo amuache. Na wakati huo hawataachana tena kwani shetani atakuwa kisha kuruka zamani.

Na ikiwa yumo katika Tahara waliyoingiliana, basi lazima angojee mpaka Tahara hiyo ishe aingie Myezini, ishe ada yake ya mwezi aingie katika Tahara. Kabla ya kuingiliana amuache. Wala hawataachana vile vile kwani shetani atakuwa ameruka zamani.

(II) *Laa Tukhrijuuhunna Min Buyuutihinna:*

Msiwatoe katika majumba yao. Yaani ukimuacha mke huna ruhusa kumtoa nyumbani. Asalie katika nyumba hiyo hiyo kwa kula na kupewa nguo mpaka eda yake ishe, kama ilivyo vile vile katika Aya ya 6 na ya 7 za Sura hii hii.

2. Basi wanapofikia muda wao, ima (warejeeni) muwaweke kwa wema, au farikianeni nao kwa wema; na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyoagizwa yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) humtengenezea njia ya kuokoka (katika kila balaa)

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ
أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا ذَوَيْ
عَدْلٍ مِّنكُمْ وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ ۚ
ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِ مَن كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ
وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَل لَّهُ
مَخْرَجًا ﴿٢﴾

3. Na humpa riziki kwa namna asiyoitazamia, (asipopatazamia). Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, Yeye humtoshea. Kwa yakini Mwenyezi Mungu anatimiza kusudi lake (lolote alitakalo; hakuna wa kumpinga). Hakika Mwenyezi Mungu amekwisha kiwekea kila kitu kipimo chake.

وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۚ وَمَن يَتَوَكَّلْ
عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ ۚ قَدْ
جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴿٣﴾

4. Na wale waliokoma na kutoka hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka (katika muda wao wa Eda), basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, na (pia ndiyo eda kwa wale) ambao hawajapata hedhi bado. Na wanawake wenye mimba eda yao ni mpaka watakapozaa. Na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) humfanyia mambo yake kuwa mepesi.

وَاللَّائِي يَئِسْنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِن نِّسَائِكُمْ
إِنِ ارْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ وَاللَّائِي لَمْ
يَحِضْنَ ۚ وَأُولَاتُ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَن
يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَل لَّهُ
مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿٤﴾

5. Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu aliyoiteremsha kwenu. Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu humfutia maovu yake na humpa ujira mkubwa.

ذَٰلِكَ أَمْرُ اللَّهِ أَنزَلَهُ إِلَيْكُمْ ۚ وَمَن يَتَّقِ
اللَّهَ يُكَفِّرْ عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُعْظِمْ لَهُ أَجْرًا ﴿٥﴾

---

Mume ndiye ajitenge chumba mbali na choo mbali. Ikiwa hapana nafasi, basi atoke yeye mume, akatafute nyumba nyingine ya kukaa mpaka ishe eda ndiyo bibi atoke na achukue vyake. Na wala hatawahi kutoka kwani pengine watakuwa wamekwisha kurejeana. Inataka awe shetani mkubwa huyo, hata muda wa miezi mitatu kuwa bado tu hajawatoka! Basi hii ndiyo *Laalla Llaaha Yuhdithu Baada Dhaalika Amraa.*

(III) *Waahsul Idda:*

Wadhibiti siku za eda ili warejeane kabla ya kumalizika.

2. Katika Aya nyingi za Sura hii Mwenyezi Mungu anawabashiria watu wa kheri kuwa watatengenekewa duniani na Akhera.

4. Zinatajwa namna za kwisha eda ya mwanamke aliyeachwa. Namna zake 5:

(a) Ikiwa kisha kupindukia myaka ya kuingia mezini. Basi eda yake humalizika mezi mitatu tangu kuwachwa.

(b) Na vile vile mwanamke mdogo asiyeingia miezini bado.

(c) Na vile vile — ulamaa wengine wansema — aliyezuwilika kabla ya wakati.

(d) Na mwenye mimba inamalizika eda yake kwa kuzaa hiyo mimba yake, japo itachukua muda mrefu kabisa au muda mfupi kabisa, japo wa papo kwa papo — baada ya kuachwa tu mara akazaa. Basi eda yake imekwisha. Anaweza kuolewa papo hapo.

(e) Ama mwanamke anayeingia miezini yeye inakwisha eda yake kwa *Thalathata Quruu* kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 228 ya *Suratul Baqarah.* Na hizi Kurui Tatu zina khitilafu. Kwa madhehebu ya Kishafii maana yake Tahara Tatu, na kwa madhehebu ya Kihanafi na Kiibadhi Hedhi Tatu.

Kwa Kishafii: Akiachwa mwanamke katika Tahara. Basi ikimalizika Tahara hiyo, ikamalizika nyingine, ikamalizika nyingine ya Tatu, basi papo hapo anaweza kuolewa.

Na kwa Kiibadhi na Kihanafi: Akiachwa katika Tahara; basi akimaliza Hedhi itakayokuja, akamaliza nyingine, akamaliza nyingine tena, ndipo eda yake itakapokwisha.

6. Wawekeni humo humo mnamokaa nyinyi, kama mpatavyo (ijapokuwa mumewawacha; maadamu eda yao haijesha). Wala msiwadhuru kwa kuwatia dhiki. Na kama wakiwa na mimba, wagharimieni mpaka wajifungue. Na kama wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao. Na shaurianeni kwa wema. Na kama mkiona udhia baina yenu, basi amnyonyeshee mwanawe (mwanamke) mwengine.

أَسْكِنُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ سَكَنتُم مِّن وُجْدِكُمْ
وَلَا تُضَارُّوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا عَلَيْهِنَّ ۚ وَإِن كُنَّ أُولَاتِ
حَمْلٍ فَأَنفِقُوا عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ فَإِنْ
أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۖ وَأْتَمِرُوا بَيْنَكُم
بِمَعْرُوفٍ ۖ وَإِن تَعَاسَرْتُمْ فَسَتُرْضِعُ لَهُ أُخْرَىٰ ﴿٦﴾

7. Mwenye wasaa agharimu kadiri ya wasaa wake; na yule ambaye amepungukiwa riziki yake, atoe katika kile alichopewa na Mwenyezi Mungu; Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu yoyote ila kwa kadiri ya alichompa. Atajaalia Mwenyezi Mungu baada ya dhiki faraji.

لِيُنفِقْ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ ۖ وَمَن قُدِرَ عَلَيْهِ
رِزْقُهُ فَلْيُنفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ ۚ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ
نَفْسًا إِلَّا مَا آتَاهَا ۚ سَيَجْعَلُ اللَّهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٧﴾

8. Na miji mingapi iliyovunja amri ya Mola wake na Mitume yake, basi tuliihisabia hisabu ngumu na tukaiadhibu kwa adhabu kali.

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ عَتَتْ عَنْ أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهِ
فَحَاسَبْنَاهَا حِسَابًا شَدِيدًا وَعَذَّبْنَاهَا عَذَابًا
نُّكْرًا ﴿٨﴾

9. Basi ikauonja ubaya wa mambo yake; na mwisho wa mambo yao ilikuwa hasara.

10. Mwenyezi Mungu aliwaandalia adhabu kali. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, mlioamini! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteremshieni Ukumbusho

فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا وَكَانَ عَاقِبَةُ أَمْرِهَا خُسْرًا ﴿٩﴾
أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ۖ فَاتَّقُوا
اللَّهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ الَّذِينَ آمَنُوا ۚ
قَدْ أَنزَلَ اللَّهُ إِلَيْكُمْ ذِكْرًا ﴿١٠﴾

11. Mtume anayekusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha (kila linalohitajiwa), ili kuwatoa wale walioamini na wakatenda mema; kuwatoa katika giza kuwapeleka katika nuru. Na anayemuamini Mwenyezi Mungu na kutenda mema atamuingiza (Mwenyezi Mungu) katika Pepo zipitazo mito mbele yake; wakae humo milele; na Mwenyezi Mungu amekwishampa riziki nzuri.

12. Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba, na ardhi kuwa mfano wa hizo. Amri (zake) zinashuka baina yao, ili mujue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kukijua (vilivyo kwa ilimu yake).

رَّسُولًا يَتْلُو عَلَيْكُمْ آيَاتِ اللَّهِ مُبَيِّنَاتٍ لِّيُخْرِجَ
الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنَ الظُّلُمَاتِ
إِلَى النُّورِ ۚ وَمَن يُؤْمِن بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا
يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ
فِيهَا أَبَدًا ۖ قَدْ أَحْسَنَ اللَّهُ لَهُ رِزْقًا ﴿١١﴾
اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ
مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ
عِلْمًا ﴿١٢﴾

اياتها ١٢ (٦٦) سورة التحريم مدنية (١٠٧) ركوعاتها ٢

Ina Aya 12 — Ina Makara 2

# SURATUT TAHRYM

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Ewe Mtume! Mbona (Kwa nini) unaharimisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu! Unatafuta radhi za wake zako (ndiyo maana ukafanya hivi)? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.

يايها النبي لم تحرم ما احل الله لك ،
تبتغي مرضات ازواجك ، والله غفور
رحيم ①

2. Hakika Mwenyezi Mungu amekupeni Sharia ya kufungua viapo vyenu; na Mwenyezi Mungu ni Mola wenu, naye ndiye Mjuzi, Mwenye hikima.

قد فرض الله لكم تحلة ايمانكم ، والله
مولىكم ، وهو العليم الحكيم ②

3. Na wakumbushe wakati Mtume alipomwambia mmoja wa wake zake jambo la siri; (na yule mkewe akalitangaza). Basi (mke yule) alipolitangaza, na Mwenyezi Mungu akamdhihirishia (Mtume wake kuwa huyu bibi ameitangaza siri) Mtume alimjuvya (huyu bibi) sehemu ya yale (aliyoyasema) na akaacha sehemu nyingine. Basi alipompasha (mkewe) habari hii, alisema (yule mkewe): "Nani aliyekupa habari hii?" (Mtume) akasema: "Amenipa habri hii yule aliye Mjuzi (wa kweli), Mwenye habari (ya kila jambo)."

واذ اسر النبي الى بعض ازواجه حديثا ،
فلما نبات به واظهره الله عليه عرف
بعضه واعرض عن بعض ، فلما نباها به
قالت من انباك هذا ، قال نباني العليم
الخبير ③

4. (Na waliokuwa na wivu zaidi katika wake zake ni Bibi Aisha na Bibi Hafsa; basi Mwenyezi Mungu aliwaambia hivi): Kama nyinyi mtatubia kwa Mwenyezi Mungu, (basi inataka mfanye upesi upesi) kwani nyoyo zenu zimemili upande kidogo. Na kama mtasaidiana juu yake (Mtume kumuudhi kwa mambo ya nyumbani, Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja naye juu yenu). Kwani Mwenyezi Mungu ni kipenzi chake, na Jibrili na Waislamu wema wote; na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia.

ان تتوبا الى الله فقد صغت قلوبكما ،
وان تظاهرا عليه فان الله هو مولىه و
جبريل وصالح المؤمنين ، والملئكة
بعد ذلك ظهير ④

---

2. Wanawake ni wanawake tu. Mtume akisema katika Hadithi zake Sahihi kuwa hakutokea mwanamke aliye kamili katika kila kitu, tangu ulimwengu ulipoanza mpaka utamalizika, isipokuwa wanawake WANE tu — Bibi Fatma na Bibi Khadija na Bibi Maryam na Bibi Asiyah. Basi hata hao wake zake Mtume walikuwa mara nyingi wakimtaabisha, hasa mabibi wawili hawa — Bibi Aysha na Bibi Hafsa — kama ilivyo katika Aya hii na ya 4. Na hawa wawili na wengine nao waliosalia, wakafanyiwa ukali katika Aya ya 5 ya Sura hii hii na katika Aya ya 28 ya *Suratul Ahzab* na penginepo. Lakini wakarejea upesi, na Mwenyezi Mungu akafurahi nao, akawapa radhi, kama ilivyo katika Aya ya 52 ya *Suratul Ahzab* na nyinginezo. Basi wakisha wale wanawake wane watukufu, na watoto wake Mtume, wanafuatia hawa wakeze Mtume.

5. (Mtume) akikupeni talaka, Mola wake atampa, badala yenu, wake wengine walio bora kuliko nyinyi; wanaofuata nguzo za Uislamu wanaoamini nguzo za Imani, watii, watubiao wanapokosa, wafanyao ibada, wafanyao mambo mengi ya kheri; waliopata kuolewa na wasiopata kuolewa.

عَسٰى رَبُّهٗۤ اِنْ طَلَّقَكُنَّ اَنْ يُّبْدِلَهٗۤ اَزْوَاجًا
خَيْرًا مِّنْكُنَّ مُسْلِمٰتٍ مُّؤْمِنٰتٍ قٰنِتٰتٍ
تٰٓئِبٰتٍ عٰبِدٰتٍ سٰٓئِحٰتٍ ثَيِّبٰتٍ
وَّاَبْكَارًا ﴿٥﴾

6. Enyi mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu, na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa amri zake; na wanatenda wanayoamrishwa (yote).

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قُوْۤا اَنْفُسَكُمْ وَاَهْلِيْكُمْ نَارًا وَّ
قُوْدُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلٰٓئِكَةٌ غِلَاظٌ
شِدَادٌ لَّا يَعْصُوْنَ اللّٰهَ مَاۤ اَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُوْنَ مَا
يُؤْمَرُوْنَ ﴿٦﴾

7. (Wataambiwa siku ya Kiama): "Enyi mliokufuru! Msilete, (msitoe) udhuru leo; bila shaka mnapewa malipo ya yale mliyokuwa mkiyatenda."

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَا تَعْتَذِرُوا الْيَوْمَ ؕ اِنَّمَا
تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٧﴾ ع ١٩

8. Enyi mlioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli; hwenda Mola wenu akakufutieni maovu yenu na kukuingizeni katika Pepo zipitazo mito mbele yake, siku ambayo Mwenyezi Mungu hatamdhalilisha Mtume wala wale walioamini pamoja naye; nuru yao itakuwa inakwenda mbele yao na pande zao za kulia (na kushoto); na huku wanasema: "Mola wetu! Tutimizie nuru yetu, na utughufirie, hakika wewe ni Mwenye uweza juu ya kila kitu."

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا تُوْبُوْۤا اِلَى اللّٰهِ تَوْبَةً
نَّصُوْحًا ؕ عَسٰى رَبُّكُمْ اَنْ يُّكَفِّرَ عَنْكُمْ
سَيِّاٰتِكُمْ وَيُدْخِلَكُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ
تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۙ يَوْمَ لَا يُخْزِى اللّٰهُ النَّبِيَّ
وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَعَهٗ ۚ نُوْرُهُمْ يَسْعٰى بَيْنَ
اَيْدِيْهِمْ وَبِاَيْمَانِهِمْ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَاۤ اَتْمِمْ لَنَا
نُوْرَنَا وَاغْفِرْ لَنَا ۚ اِنَّكَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٨﴾

9. Ewe Nabii! Shindana na makafiri na wanafiki na uwe mgumu kwao; na makazi yao ni Jahanamu; nayo ni marejeo mabaya kabisa.

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ جَاهِدِ الْكُفَّارَ وَالْمُنٰفِقِيْنَ وَاغْلُظْ
عَلَيْهِمْ ؕ وَمَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿٩﴾

10. Mwenyezi Mungu amepiga (anapiga) mfano wa wale wabaya waliokufuru, ni mkewe Nuhu na mkewe Luti. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili hao miongoni mwa waja wetu (wema); lakini (wanawake hao), waliwafanyia hiana (waume zao watukufu hao), na (waume zao hao) hawakuweza kuwasaidia chochote mbele ya Mwenyezi Mungu na ikasemwa: "Uingieni Moto pamoja na hao wanaouingia."

ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوا امْرَاَتَ نُوْحٍ وَّامْرَاَتَ
لُوْطٍ ؕ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَالِحَيْنِ
فَخَانَتٰهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا
وَّقِيْلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ الدّٰخِلِيْنَ ﴿١٠﴾

11. Na Mwenyezi Mungu amepiga, (anapiga) mfano wa wale walioamini kweli, ni mkewe Firauni.

وَضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا امْرَاَتَ
فِرْعَوْنَ ۘ اِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِيْ عِنْدَكَ

---

6. Wanalazimishwa wakubwa wawatengeneze walio chini yao au yatawafika na wao maafa yatakayowafika hao kwani wao ndio waendeshaji wao.

10. Hapa inabainishwa kuwa wabaya hawatapata salama kwa ajili ya watu wema waliokuwa pamoja nao, kama tulivyobainisha katika Aya ya 46 ya *Surat Hud* na nyinginezo.

11. Na hapa inabainishwa kuwa watu wema haitawafika balaa itakayo wafika watu wao walio wabaya. Kila

(Mumewe kafiri kubwa namna hilo, na yeye Mwislamu mzuri namna hivyo). (Wakumbusheni watu) aliposema "Ee Mola wangu! Nijengee nyumba Peponi karibu yako, na uniokoe na Firauni na amali zake (mbovu), na niokoe na watu madhalimu."

بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِنْ فِرْعَوْنَ
وَعَمَلِهِ وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِينَ ﴿١١﴾

12. Na Mariamu mtoto wa Imrani aliyejihifadhi nafsi yake na tukampulizia humo roho yetu, (inayotokana na sisi) na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na Vitabu vyake; na alikuwa miongoni mwa wanyenyekevu (wakubwa).

وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرٰنَ الَّتِيٓ أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا
فَنَفَخْنَا فِيهِ مِنْ رُّوحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمٰتِ
رَبِّهَا وَكُتُبِهِ وَكَانَتْ مِنَ الْقٰنِتِينَ ﴿١٢﴾ ع ٢

---

mtu atalipwa kwa amali zake. Cha kulipwa watu wema na wabaya ni AMALI si UJAMAA.

11-12. Katika maelezo ya hapa wamepachikiapachikia ili wampatie Utume huyo mtu wao. Mahala pa mwisho tulipotaja ukafiri wa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad ni katika Aya ya 40 ya *Suratul Ahzaab*.

ركوعاتها ٢ (٦٧) سُورَةُ الْمُلْكِ مَكِّيَّة (٦٧) اٰيَاتُهَا ٣٠

*Ina Aya 30* *Ina Makara 2*

# SURATUL MULK

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Ametukuka yule ambaye Mkononi mwake umo ufalme (wote); Naye ni mwenye uweza juu ya kila kitu.

تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

2. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Msamaha;

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٢﴾

3. Ambaye ameumba mbingu saba zilizo tabakatabaka, (moja juu ya moja); huoni tafauti yoyote katika uumbaji wa Mwingi wa rehema. Hebu rudisha macho (yako uzidi kutazama); je unaona kosa?

الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۖ مَا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَٰنِ مِنْ تَفَاوُتٍ ۖ فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِنْ فُطُورٍ ﴿٣﴾

4. Tena rudisha macho (yako) mara nyingi zaidi; jicho lako litarudia hali ya kuwa limehizika na umechoka.

ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ إِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٤﴾

5. Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu hii kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapigia mashetani; na Tumewawekea tayari adhabu ya Moto uwakao (kwa nguvu).

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيَاطِينِ ۖ وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابَ السَّعِيرِ ﴿٥﴾

6. Na kwa waliomkufuru Mola wao iko adhabu ya Jahanamu (inawangojea). Na ni marejeo mabaya yaliyoje!

وَلِلَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٦﴾

7. Watakapotupwa humo watasikia rindimo (mngurumo) lake, na hali ya kuwa inafoka

إِذَا أُلْقُوا فِيهَا سَمِعُوا لَهَا شَهِيقًا وَهِيَ تَفُورُ ﴿٧﴾

8. Unakaribia kupasuka kwa hasira (yake juu ya wabaya). Kila mara litakapotupwa humo kundi (la wabaya) walinzi wake watawauliza: "Je! Hakukufikieni Mwonyaji?

تَكَادُ تَمَيَّزُ مِنَ الْغَيْظِ ۖ كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٨﴾

---

1. Sura hii Mtume alikuwa anapenda kila mtu awe anayaweka machoni madhumuni ya Aya zake, kama alivyoitaja Hadithi hii Imam Attabarany na Imam Abd bin Humeid na wengineo. Na Mtume alikuwa ana dasturi ya kuisoma kila usiku kabla ya kulala, kama alivyotaja Imam Attirmdhy na wengineo. Yote ni makumbusho ya uweza na neema za Mungu.

Anaona mtu humu kuwa mambo yote yamo katika mkono wa Mwenyezi Mungu, kwa hivyo amuabudu Yeye amuombe Yeye na amtegemee Yeye tu basi.

Mambo yote ni ya Mungu — Atakalo ndilo huwa
Ndiye Pweke mwenye quwa — Mwenye amri na shani.